**KIZIDUO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA TATU KWA MWAKA WA FEDHA (2021/2022) CHA KAMATI YA UTEKELEZAJI YA WILAYA (CMT) KILICHOFANYIKA TAREHE 20 OKTOBA, 2021.**

**MUHTASARI NAMBA: CMT 03/2020/2021.**

**WALIOHUDHURIA:-**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ndg | Hemed S. Magaro | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Mwenyekiti |
| 2. | " | Elizabeth Ngobei | Afisa Utumishi (W) | Katibu |
| 3. | " | Jacob Makala | Afisa Elimu Sekondari (w) | " |
| 4. | " | Christopher Nyaki | Mweka Hazina (W) | " |
| 5. | " | Sondo Mrua Dotto | Kaimu Mdhibiti Ubora (W) | " |
| 6. | " | Edna J. Lukuta | Mwanasheria (W) | " |
| 7. | " | Ludao William | Kny: Afisa Tehama (W) | " |
| 8. | " | Oresta Kapinga | Kny:Afisa Mipango (W) | " |
| 9. | " | Karugutu Zuberi | Afisa Elimu Msingi (W) | " |
| 10. | " | Ashura Kang'ombe | Afisa Ugavi (W) | " |
| 11. | " | Shabani A Kigumi | Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika(W) | " |
| 12. | " | Laurent Keegan | Afisa Utamaduni | " |
| 13. | " | Emmanuel Mzile | Mhasibu wa Mapato | " |
| 14. | " | Robert Nigangwa | Mratibu wa CHF | " |
| 15. | " | Godlisten Masanja | Kny: Afisa Usafirishaji | " |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 16. | " | Jesca Majanja | Kny: Maliasili na Ardhi (W) | " |
| 17. | " | Kletus Mbawala | Kny: Afisa Maendeleo ya Jamii (w) | " |
| 18. | " | Kalunde Shabani | Kaimu Katibu TSC (W) | " |
| 19. | " | Karim Msomoka | Kny: Mhasibu wa Matumizi | " |
| 20. | " | Florence Mahimbo | Mhasibu | " |
| 21. | " | Issa Mwaisyula | Afisa Biashara | " |
| 22. | " | Masanja Manane | Kaimu: Mganga Mkuu (w) | " |
| 23. | " | Dr Kija Maige | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) | " |
| 24. | " | Amos Wigayi | Afisa Uchaguzi (W) | " |
| 25. | " | Chrispo Kisoma | Kaimu Afisa Nyuki (w) | " |
| 26. | " | Kivaria C. Mshana | Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (w) | " |
| 27. | " | Moses Barton | Kny: Afisa Usafi na Mazingira (w) | " |
| 28. | " | Stanley Ugulumo | Afisa Ushirika | " |
| 29. | " | Anold Moshi | Mkaguzi wa Ndani (W) | " |

**SEKRETARIETI**

1. " Noel Benjamini
2. " Godlisten Masanja

**AGENDA NA: CMT 03/2020/2021/1. KUFUNGUA KIKAO.**

Baada ya kujiridhisha na akidi, Mwenyekiti alifungua kikao saa 07:01 mchana kwa kuwashukuru Wajumbe na kuwakaribisha kuchangia Agenda zilizowasilishwa katika Kikao hicho.

**AGENDA NA: CMT 03/2020/2021/2. KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO.**

Jumla ya Agenda kumi na tatu **(13)** ziliidhinishwa ili ziweze kujadiliwa na Wajumbe. Agenda hizo ni kama zinavyoonekana hapa chini:-

| AGENDA NAMBA | MAELEZO YA AGENDA |
|---|---|
| 1 | Kufungua kikao |
| 2 | Kuridhia Agenda |
| 3 | Kusoma na kuthibitisha Mihtasari wa kikao cha CMT |

4 Yatokanayo ya CMT

5 Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa Mwezi Julai hadi Septemba 2021/2022

6 Taarifa ya Maendeleo ya ukusanyaji wa Mapato katika vyanzo vidogo vidogo kwa Mwezi Septemba 2021/2022.

7 Taarifa ya Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2021.

8 Taarifa ya Utendaji Kazi wa Idara zinazoripoti kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.

9 Maombi ya Tsh 15,845,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Vyoo katika shule ya Msingi Bukala.

10 Ombi la kuongeza walinzi wanne wa kampuni za ulinzi.

11. Mpango wa ujenzi wa vyumba vya madarasa na Afya kwa fedha za UVIKO 19 TSHS . **3,664,155,217.04**

12 Mengineyo

13 Kufunga kikao

**AGENDA NA: CMT 03/2020/2021/3 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 15 SEPTEMBA, 2021.**

Muhtasari wa Kikao cha tarehe 15 Septemba, 2021, ulisomwa, ambapo Wajumbe waliafiki kuwa yote yaliyomo kwenye Muhtasari huo ndio waliyoyajadili na kuyatolea maamuzi, hivyo kutoa idhini kwa Mwenyekiti na Katibu kusaini Muhtasari huo kwa niaba ya wajumbe wote ili uweze kuwa kumbukumbu halali ya Kikao hicho.

**AGENDA NA: CMT 03/2020/2021/11. MPANGO WA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA NA AFYA KWA FEDHA ZA UVIKO 19 TSHS . 3,664,155,217.04**

Agenda hii iliwasilishwa na Afisa Mipango ambapo aliijulisha Kamati kwamba, Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ilipokea fedha kiasi cha Tshs.3,664,155,217.04, kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa vyumba 123 vya madarasa kwa shule 27 za sekondari kwa thamani ya TSHS.2,460,000,000,madarasa 55 katika shule shikizi 23 kwa thamani ya TSHS.1,100,000,000.Ujenzi wa nyumba za watumishi kwa thamani ya TSHS. 90,000,000 .Mafunzo,ufuatiliaji na tathimini kiasi cha Tshs. 14,155,217.04 kupitia Fedha za Mkopo

Nafuu wa Shirika la Fedha Duniani (IMF). Aidha Menejimenti iliijulisha kamati kwamba kiasi cha shilingi 14,155,217.04 zilizotengwa kwa ajili ya ufuatiliaji na tathimini haziwezi kukidhi mahitaji halisi ya ufuatiliaji wa miradi hii

**Mapendekezo ya Kamati**

Kamati iliridhia na kukbaliana kwamba ni vema tupeleke mapendekezo kwenye Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kwamba miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ifanyike kwa mfumo wa nguvu jamii (FORCE ACCOUNT) kwa kuzingatia changamoto ya mtawanyiko wa miradi ambayo itatekelezwa kwa Halmashauri nzima. Aidha kwa upande wa nyumba ya Mtumishi Idara ya Afya ni vema tupendekeze matumizi ya Mkandarasi.

**AGENDA NA: CMT 03/2020/2021/11 MATANGAZO.**

Kwenye Kikao cha tarehe 20 Oktoba 2021 hapakuwepo na mengineyo yaliyowasilishwa kwenye meza ya Mwenyekiti aidha kwa njia ya maandishi au kwa hoja ya moja kwa moja

**AGENDA NA: CMT 03/2020/2021/12 KUFUNGA KIKAO.**

Kabla ya kufunga kikao, Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kwamba, Wakuu wa Idara wote wanapaswa kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa kwenye kikao cha kamati ya utekelezaji kwa lengo kuwa katika kikao kijacho yawe yametekelezwa na baada ya maelezo hayo Mwenyekiti alifunga Kikao saa 08:31 mchana.

| | |
|---|---|
| **M U H T A S A R I** | **U M E T H I B I T I S H W A** |
| Ngobei | |
| **Ndg. Elizabeth Ngobei** | **Ndg. Hemed S. Magaro** |
| Afisa Utumishi (W) | Mkurugenzi Mtendaji (W) |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |

27/OCTOBA/2021

**TAREHE.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KWA MWAKA (2020/2021) KILICHOKETI TAREHE 27 OCTOBA, 2021.
## MUHTASARI NAMBA: TB: 4/2020/2021

**WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Dr. Kija A. Maige | Afisa Mifugo na Uvuvi (W) | Mwenyekiti |
| 2. Ashura H. Kang'ombe | Afisa ugavi (W) | Katibu |
| 3. Edna Lukuta | Mwanasheria | Mjumbe |
| 4. Dastan Kamuzola | Afisa Tehama | Mjumbe |
| 5. Elizabeth Ngobei | Afisa Utumishi | Mjumbe |
| 6. Jenifer Temu | Afisa Mipango | Mjumbe |
| 7. Dr. Wilfred Rwechungura | Mganga Mkuu | Mjumbe |

**B. SEKRETARIETI.**

1. Godlisten Masanja

**AGENDA NA: TB 04/2020/2021/01. KUFUNGUA KIKAO**

Baada ya kujiridhisha na akidi, Mwenyekiti alifungua Kikao saa 12:51 Mchana, kwa kuwataka Wajumbe wajielekeze kwenye mjadala mzima wa agenda ambazo ziliwasilishwa mbele yao.

**AGENDA NA: TB 04/2020/2021/02. KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO.**

Jumla ya Agenda saba **(7)** ziliridhiwa ili zijadiliwe. Agenda hizo ni:-

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda za Kikao
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 9 Julai, 2021.
4. Kuridhia ujenzi wa miradi ya COVID kwa kutumia mafundi wasiokuwa wakandarasi (ujenzi wa force)
5. Mengineyo.
6. Kufunga Kikao.

**AGENDA NA: TB 04/2020/2021/3 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 9 Julai, 2021.**

Muhtasari wa Kikao kilichofanyika tarehe 9 Julai, 2020, ulisomwa, ambapo Wajumbe waliafiki kuwa, yote yaliyomo kwenye Muhtasari huo ndio waliyoyajadili na kuyatolea maamuzi. Kuthibitisha hayo, Mwenyekiti na Katibu waliweka saini zao kwa niaba ya wote, ili Muhtasari huo uwe kumbukumbu halali wa Kikao hicho.

**AGENDA NA: TB 04/2020/2021/4 KUPITISHA MANUNUZI NA UJENZI WA MIRADI YA MADARASA YA SEKONDARI NA MSINGI NA MIRADI YA AFYA YA UVIKO KWA KUTUMIA MAFUNDI WASIOKUWA WAKANDARASI (FORCE ACCOUNT) YENYE GHARAMA TSHS. 3,650,000,000.00**

Katibu aliwaeleza majumbe kuwa kuna fedha imepokelewa za COVID 19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya sekondari 123, madarasa ya shule shikizi 55 na ujenzi wa nyumba ya mtumishi (Three in one) moja katika Zahanati ya Mbeya. Hivyo aliwaomba wajumbe waridhie miradi hiyo ikatekelezwe kwa kutumia mafundi wasiokuwa wakandarasi (Force Account) kwa kuwa hayo ni matakwa ya mfadhili wa miradi.

**AZIMIO**

Wajumbe walikubaliana kwa Pamoja na kuridhia kuwa kazi hiyo ikafanyika kwa kutumia mafundi wasiokuwa wakandarasi (Force Account) na wajumbe walishauri kuwa ni vizuri miradi hii itambulishwe haraka kwenye ngazi za huko shuleni ili miradi iweze kutekelezwa kwa wakati

**AGENDA NA:TB 04/2019/2020/5. MENGINEYO.**

**Hakukuwa na mengineyo**

.

**AGENDA NA:TB 04/2019/2020/6. KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga Kikao saa 08:20 mchana na alitumia fursa hiyo kuwashukuru Wajumbe kwa michango yao.

| **M U H T A S A R I** | **U M E T H I B I T I S H W A** |
|---|---|
| ............................ | ............................ |
| **Ashura H. Kang'ombe** | **DR KIJA MAIGE** |
| KATIBU WA BODI YA ZABUNI | MWENYEKITI WA BODI YA ZABUNI |

.......27/10/2021.......

**TAREHE.**